# BENKI KUU YA TANZANIA




## Tathmini Ya Mwendo Wa Uchumi

Agosti 2026

# Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ....................1
2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa .................... 3
2.1 Mfumuko wa Bei .................... 3
2.2 Sera ya Fedha .................... 5
2. 3 Viwango vya Riba .................... 7
2.4 Masoko ya Fedha .................... 7
2. 5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali .................... 9
2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa .................... 9
2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje ....................11
3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar .................... 14
3.1 Mfumuko wa Bei .................... 14
3.2 Bajeti ya Serikali .................... 15
3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje .................... 16
Viambatisho .................... 18
Tafsiri ya Dhana Muhimu .................... 31

## 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Taarifa ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Julai 2026, inaonesha uchumi wa dunia kwa mwaka 2026 kukua kwa asilimia 3, licha ya kukabiliwa na mivutano ya kijiografia. Ukuaji huo unatarajiwa kutofautiana kikanda. Pamoja na sababu nyingine, mabadiliko ya mara kwa mara ya bei za nishati na utofauti wa matumizi ya teknolojia ya akili unde katika mnyororo wa ugavi wa dunia vimeendelea kusababisha tofauti hizo. Pamoja na sababu hizo, fahirisi za viwango vya kutotabirika kwa sera za uchumi wa dunia na biashara kimataifa zilishuka zaidi mwezi Julai 2026 (Kielelezo 1.1a na Kielelezo 1.1b).

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutotabirika kwa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutotabirika kwa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

Bei za bidhaa katika soko la dunia hazikuwa tulivu. Bei za mafuta ghafi zilishuka mwanzoni mwa mwezi Julai 2026 kufuatia kutiwa saini kwa hati ya makubaliano kati ya Marekani na Iran mwezi Juni 2026, kabla ya kuanza kupanda tena katikati ya mwezi Julai kutokana na kurejea kwa mashambulizi ya meli za mafuta katika mlango Bahari wa Hormuz. Hata hivyo, fahirisi ya bei za nishati ilipungua kwa asilimia 1.1, ikichangiwa na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi na makaa ya mawe. Kwa wastani bei ya mafuta ghafi ilipungua kwa asilimia 2.3 hadi kufikia dola za Marekani 79.80, kutoka dola za Marekani 81.70 kwa pipa mwezi Juni 2026.

Kwa upande mwingine, athari za kupungua kwa bei za mafuta ghafi zilifidiwa kwa kiasi na ongezeko la asilimia 19.1 ya bei ya gesi asilia barani Ulaya. Aidha, bei ya mafuta ghafi iliendelea kubaki juu kwa asilimia 28.5 ikilinganishwa na wastani wa dola za Marekani 62.1 kwa pipa iliyorekodiwa robo ya nne ya mwaka 2025 kabla ya mgogoro wa kivita, na hivyo kuendelea kuweka msukumo kwenye gharama za maisha, hasa kwa nchi zinazoagiza nishati kutoka nje.

Bei ya dhahabu ilifikia wastani wa dola za Marekani 4,073 kwa wakia ikipungua kutoka dola za Marekani 4,228 kwa wakia mwezi Juni 2026, kutokana na kupungua kwa mahitaji ya dhahabu kama hifadhi salama ya thamani kuanzia mwanzoni mwa mwezi Julai 2026. Bei ya mafuta ya mawese, kwa kiasi kikubwa ilibaki karibu na kiwango chake cha awali, ikifikia dola za Marekani 1,101 kwa tani ikiakisi kupungua kwa matumizi ya mafuta hayo katika uzalishaji wa biodizeli.

Bei za mbolea ziliendelea kuwa na mwenendo tofauti, ambapo bei ya mbolea aina ya DAP ilibaki thabiti kwa dola za Marekani 781.3 kwa tani huku mbolea ya UREA ikishuka kwa asilimia 11.7 hadi dola za Marekani 400 kwa tani, hali iliyosaidia kupunguza gharama za pembejeo za kilimo.

Kwa ujumla, wastani wa bei za bidhaa za chakula ulipungua kwa asilimia 0.3. Hata hivyo, bei ya ngano iliongezeka kwa asilimia 8.4, kufuatia kuibuka kwa wasiwasi mpya kuhusu ugavi kutoka maeneo makubwa ya uzalishaji duniani. Bei ya sukari katika soko la dunia iliongezeka kwa asilimia 6.2. Bei ya kahawa ikiongezeka kwa kasi, ambapo bei ya kahawa aina ya Arabika na Robusta ziliongezeka kwa asilimia 16.5 na 9.1, mtawalia. Ongezeko hilo lilichangiwa na matarajio ya kupungua kwa ugavi, hususan nchini Brazil na Vietnam (Kielelezo 1.2, Jedwali 1.1 na Kiambatisho A8).

**Kielelezo 1.2: Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia**




Chanzo: Bloomberg

**Jedwali 1.1: Bei ya Bidhaa Katika Soko la Dunia**

Wastani kwa kila mwezi

| Bidhaa | Kizio | Jun-26 | Jul-26 | Mabadiliko (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mafuta ghafi, wastani | Dola za Marekani/pipa | 81.7 | 79.8 | -2.3 |
| Dhahabu | Dola za Marekani/wakia | 4,228 | 4,073 | -3.7 |
| Gas asilia, Ulaya | Dola za Marekani/MMBtu | 15.17 | 18.06 | 19.1 |
| Ngano, Marekani HRW | Dola za Marekani/tani | 286 | 310 | 8.4 |
| Sukari, Dunia | Dola za Marekani/kg | 0.32 | 0.34 | 6.2 |
| Kahawa , Arabika | Dola za Marekani/kg | 6.79 | 7.91 | 16.5 |
| Kahawa, Robusta | Dola za Marekani/kg | 3.73 | 4.07 | 9.1 |
| Mafutaya Mawese | Dola za Marekani/tani | 1,104 | 1,101 | -0.3 |
| DAP | Dola za Marekani/tani | 783.8 | 781.3 | -0.3 |
| Urea | Dola za Marekani/tani | 453.1 | 400 | -11.7 |

Chanzo: Bloomberg

Mfumuko wa bei duniani uliendelea kubaki katika viwango vya juu. Nchini Marekani, mfumuko wa bei wa jumla ulipungua miezi miwili mfululizo na kufikia asilimia 3.4, kutoka asilimia 3.5 mwezi Juni 2026. Katika ukanda wa Umoja wa Ulaya, mfumuko wa bei uliongezeka hadi asilimia 2.9 kutoka asilimia 2.8, hivyo kubakia juu ya lengo la asilimia 2 la Benki Kuu ya Ulaya. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mfumuko wa bei wa nishati wa asilimia 10, pamoja na mfumuko wa bei wa huduma wa asilimia 3.3.

Nchini China, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 0.5 kutoka asilimia 1, ikiwa ni kiwango cha chini zaidi tangu Januari 2026. Hali hiyo ilitokana na kuendelea kushuka kwa bei za chakula, jambo lililoongeza wasiwasi wa shinikizo la mfumuko wa bei hasi.Nchini India, mfumuko wa bei uliendelea kubaki katika kiwango cha chini cha asilimia 4.5, na kuwa ndani ya wigo wa lengo la Benki Kuu ya India wa asilimia 2 hadi 6 (Kielelezo 1.3).

Kwa ujumla, benki kuu za nchi nyingi ziliendelea kuwa na mwelekeo wa tahadhari katika utekelezaji wa sera ya fedha, zikihofia uwezekano wa kuendelea kwa athari za awamu ya pili zinazotokana na kuongezeka kwa gharama za nishati pamoja na kuendelea kuwepo kwa mfumuko wa bei wa huduma katika viwango vya juu.

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi**

Asilimia



Chanzo: Bloomberg

Mfumuko wa bei katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), uliendelea kuwa na mwenendo mchanganyiko, huku nchi nyingi zikiendelea kubaki ndani ya vigezo vya utangamano vya kikanda vilivyokubaliwa (Kielelezo 1.4 na Kielelezo 1.5).

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.5: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**

Asilimia



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei ulibaki ndani ya lengo la kitaifa pamoja na vigezo vya mtangamano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika(SADC), ingawa ulikuwa juu ya wastani kihistoria. Mfumuko wa bei wa jumla wa mwaka uliongezeka hadi asilimia 4.2 mwezi Julai 2026, kutoka asilimia 4.0 mwezi uliotangulia na asilimia 3.3 mwezi Julai 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.1). Ongezeko hili lilisababishwa zaidi na kuongezeka kwa bei za mafuta kwenye gharama za usafirishaji. Ingawa mivutano ya kijiografia imeendelea kufanya makisio ya mfumuko wa bei katika kipindi cha muda mfupi kuwa hatarini kwa mishtuko ya nje, bei za vyakula ambazo zimeendelea kuwa chini, zinatarajiwa kuendelea kupunguza shinikizo la ongezeko la bei za bidhaa na huduma kwa walaji.

**Jedwali 2.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

2020 = 100

| | | Badiliko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiliko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 |
| Vyakula na vinywaji baridi | 28.2 | -0.8 | -0.7 | -0.8 | 7.6 | 4.1 | 4.1 |
| Vinywaji vikali na tumbaku | 1.9 | 0.1 | -0.1 | 0.2 | 3.0 | 1.9 | 1.9 |
| Nguo, mavazi na viatu | 10.8 | 0.0 | 0.0 | 0.2 | 1.9 | 1.3 | 1.6 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | -0.4 | 0.7 | 0.0 | 1.3 | 1.2 | 1.6 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi | 7.9 | 0.6 | 0.0 | 0.4 | 2.4 | 2.5 | 2.2 |
| Afya | 2.5 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 1.6 | 1.3 | 1.4 |
| Usafiri | 14.1 | 0.0 | 1.6 | 0.1 | 1.2 | 13.6 | 13.8 |
| Habari na mawasiliano | 5.4 | 0.0 | 0.0 | -0.3 | 0.2 | 0.9 | 0.6 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.6 | -0.1 | -0.2 | 0.0 | 1.0 | 0.5 | 0.7 |
| Elimu | 2.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 3.1 | 2.7 | 2.8 |
| Migahawa na huduma za malazi | 6.6 | 0.0 | 0.0 | 0.8 | 1.0 | 1.9 | 2.7 |
| Bima na huduma za kifedha | 2.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.6 | 0.2 | 0.2 |
| Huduma binafsi, hifadhi ya jamii na bidha na huduma mchanganyiko | 2.1 | 0.0 | 0.1 | -0.1 | 2.0 | 3.6 | 3.4 |
| Fahirisi bidhaa zote | 100.0 | -0.3 | 0.1 | -0.1 | 3.3 | 4.0 | 4.2 |
| Makundi mengine teule | | | | | | | |
| Faharisi ya bidhaa za msingi | 73.9 | 0.1 | 0.3 | 0.2 | 1.9 | 3.7 | 3.9 |
| Fahirisi isiyojumuisha fahirishi za bidhaa za msingi | 26.1 | -1.1 | -0.4 | -1.1 | 7.1 | 4.8 | 4.9 |
| Fahirisi za mafuta, nishati na bili za maji | 5.7 | -1.3 | 1.5 | -0.8 | 1.0 | 6.3 | 6.9 |
| Fahirisi za huduma | 37.2 | 0.0 | 0.7 | 0.4 | 0.8 | 5.4 | 5.7 |
| Fahirisi za bidhaa | 62.8 | -0.4 | -0.2 | -0.4 | 4.7 | 3.3 | 3.3 |
| Fahirisi za bidhaa na huduma za elimu | 4.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 2.8 | 1.6 | 1.7 |
| Fahirisi za bidhaa zote isipokuwa chakula na vinywaji visivyo na kilevi | 71.8 | 0.0 | 0.5 | 0.2 | 1.5 | 4.0 | 4.2 |

Chanzo: Ofisi ya taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa Bei na Malengo yake**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei wa bidhaa za msingi, usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa na nishati, uliongezeka na kufikia asilimia 3.9 mwezi Julai 2026, kutoka asilimia 3.7 mwezi Juni 2026, ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwezi Julai

2025 (Kielelezo 2.1.2). Ongezeko hili linaakisi kupanda kwa gharama za usafirishaji (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.4).

**Kielelezo 2.1.2: Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Miezi Kumi na Mbili**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei za vyakula wa mwaka ulikuwa asilimia 4.1 mwezi Julai 2026, sawa na kiwango cha mwezi Juni 2026, na chini ya asilimia 7.6 ya mwezi Julai 2025 (Jedwali 2.1.1). Kupungua huku kuliakisi ongezeko la upatikanaji wa chakula kufuatia kuendelea kwa msimu wa mavuno, ambapo bei za jumla za mahindi, mchele, maharage na mtama zilikuwa chini ya viwango vya mwezi Julai 2025 (Kielelezo 2.1.3a na Kielelezo 2.1.3b).

**Kielelezo 2.1.3: Mabadiliko ya Mwaka ya Bei za Jumla za Mazao**

**a. Mazao ya Vyakula Vikuu**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**b. Mazao ya Vyakula Mbadala**

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya chakula inayohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) iliendelea kuwa ya kutosha, ikifikia tani 479,065. Kiwango hiki ni cha juu zaidi ya kigezo cha kitaifa cha angalau tani 150,000. Tani 3,008.5 za mahindi na mpunga zilitolewa kwa wafanyabiashara mwezi Julai 2026 (Jedwali 2.1.2).

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula Iliyohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

Tani

| Kipindi | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 | 567,469 |
| Feb | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 | 560,008 |
| Mac | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 | 533,634 |
| Apr | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 | 510,927 |
| Mei | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 | 496,576 |
| Jun | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 | 480,219 |
| Jul | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 | 479,065 |
| Ago | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 | |
| Sep | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 | |
| Okt | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 | |
| Nov | 147,401 | 244,223 | 702,502 | 590,425 | |
| Des | 137,655 | 248,282 | 677,115 | 577,376 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

Mfumuko wa bei ya nishati, mafuta na bili za maji uliongezeka hadi asilimia 6.9 mwezi Julai 2026, kutoka asilimia 6.3 mwezi Juni 2026 na asilimia 1.0 mwezi Julai 2025 (Jedwali 2.1.1 na Kielelezo 2.1.2). Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei ya mafuta ya taa. Bei za petroli na dizeli zilipungua kwa kiasi.

**Kielelezo 2.1.4: Bei za Bidhaa za Mafuta**

Kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za dunia

Mfumuko wa bei za msingi uliendelea kuwa na mchango mkubwa kwenye mfumuko wa bei wa jumla, ukichangia asilimia 2.9 kwenye kiwango cha asilimia 4.2 cha mfumuko wa bei wa jumla cha mwezi Julai 2026 (Kielelezo 2.1.5).

**Kielelezo 2.1.5: Mchango Katika Mfumuko wa Bei**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## 2.2 Sera ya Fedha

Mwezi Julai 2026, Kamati ya Sera ya Fedha iliongeza kiwango cha Riba ya Benki Kuu kutoka asilimia 5.75 hadi asilimia 6.25 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2026. Hatua hiyo ililenga kudhibiti shinikizo la mfumuko wa bei lililoanza kujitokeza, ikiwemo uwezekano wa kutokea kwa athari za awamu ya pili zinazotokana na kuendelea kuwepo kwa gharama kubwa za nishati, mbolea na usafirishaji.

Kutokana na mabadiliko hayo, utekelezaji wa sera ya fedha ulirekebishwa ili kuhakikisha kiwango cha riba katika soko la fedha baina ya mabenki cha siku saba kinaendelea kubaki ndani ya wigo wa asilimia 4.75 kwa kiwango cha chini na asilimia 7.75 kwa kiwango cha juu cha riba ya Benki Kuu.

Ili kuendana na uamuzi wa kamati ya sera ya fedha, shughuli za utekelezaji wa sera ziliendelea kuhakikisha kuwa kuna ukwasi wa kutosha katika sekta ya benki, ambapo wastani wa riba ya siku saba ya soko la fedha baina ya mabenki uliendelea kuwa sawia na kiwango cha Riba ya Benki Kuu (Kielelezo 2.2.1). Usimamizi wa ukwasi ulifanyika kupitia mikopo ya muda mfupi (reverse repos) kwa mabenki (Kielelezo 2.2.2).

**Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na Wastani wa Siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya Muda Mfupi Kwa Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa asilimia 26.9 katika mwaka ulioishia Julai 2026, juu kidogo ya asilimia 25.5 ya mwezi Juni 2026 (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Ukuaji huu ulichagizwa zaidi na mikopo kwa sekta binafsi, ambayo iliongezeka kwa asilimia 31.2 ikilinganishwa na asilimia 28.1 mwezi Juni 2026 (Kielelezo 2.2.4 na Kielelezo 2.2.5).

Uimara wa ukuaji wa mikopo unaakisi kuendelea kuimarika kwa mahitaji ya mikopo sambamba na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi, ikiwemo ununuzi wa mazao wakati wa msimu wa mavuno. Aidha, ongezeko la kiwango cha Riba ya Benki Kuu kilichoanza kutumika mwezi Julai 2026 kinatarajiwa kupunguza kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo katika uchumi. Hata hivyo, athari za hatua hiyo zinatarajiwa kujitokeza baada ya muda.

**Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi Wa Fedha**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake**

| | Kiasi (Shilingi Bilioni) | | | Ukuaji kwa mwaka (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipengele | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 |
| Rasilimali halisi za nje | 15,726.1 | 13,449.0 | 14,646.0 | 28.6 | -13.3 | -6.9 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 13,884.0 | 13,077.5 | 14,562.1 | 13.5 | -4.0 | 4.9 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,842.1 | 371.6 | 83.9 | --- | -80.3 | -95.4 |
| Rasilimali halisi za ndani | 40,565.0 | 56,170.4 | 56,763.8 | 16.9 | 40.5 | 39.9 |
| Madai rasmi ya ndani | 52,548.3 | 65,928.9 | 65,896.2 | 11.2 | 26.4 | 25.4 |
| Dhamana za Serikali zilizonunuliwa na benki za biashara | 7,961.4 | 11,247.8 | 11,569.6 | -6.0 | 40.8 | 45.3 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 40,972.2 | 51,923.1 | 53,773.6 | 15.9 | 28.1 | 31.2 |
| Rasilimali nyinginezo | -11,983.4 | -9,758.5 | -9,132.4 | -4.5 | -19.8 | -23.8 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 56,291.1 | 69,619.4 | 71,409.8 | 19.9 | 25.5 | 26.9 |
| Amana za fedha za kigeni | 13,653.2 | 15,365.4 | 16,771.0 | 19.2 | 11.6 | 22.8 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 42,637.9 | 54,254.1 | 54,638.9 | 20.2 | 30.1 | 28.1 |
| Amana zinginezo | 16,406.3 | 19,982.0 | 19,984.5 | 23.3 | 24.4 | 21.8 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 26,231.6 | 34,272.0 | 34,654.4 | 18.3 | 33.6 | 32.1 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzunguko | 8,122.1 | 8,824.5 | 8,933.6 | 14.6 | 12.1 | 10.0 |
| Amana za hundi | 18,109.4 | 25,447.5 | 25,720.8 | 20.0 | 43.1 | 42.0 |
| Fedha za msingi (M0) | 13,423.8 | 16,738.8 | 16,188.3 | 23.2 | 34.4 | 20.6 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko Katika Vyanzo vya Ujazi wa Fedha kwa Mwaka**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.5: Mwenendo Wa Mikopo Kwa Sekta Binafsi**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Mikopo kwa sekta binafsi iliendelea kuwa na mgawanyo mpana katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sekta ya uchukuzi na mawasiliano ilirekodi ukuaji mkubwa zaidi kwa mwaka, ikifuatiwa na sekta ya uchimbaji madini na mawe, pamoja na biashara (Jedwali 2.2.2).

Mikopo binafsi, ambayo kwa kiasi kikubwa ilielekezwa kwenye shughuli ndogo sana, ndogo na za kati, iliendelea kuchukua sehemu kubwa zaidi ya mikopo ya benki kwa asilimia 34, ikifuatiwa na sekta ya biashara na kilimo kwa asilimia 15.4 na asilimia 14, mtawalia (Kielelezo 2.2.6).

**Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia

| | Jul-25 | Sep-25 | Des-25 | Mac-26 | Jun-26 | Jul-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchukuzi na mawasiliano | 18.9 | 17.4 | 29.4 | 39.5 | 59.5 | 66.0 |
| Uchimbaji Madini | 0.8 | 32.4 | 91.1 | 78.4 | 39.9 | 65.2 |
| Biashara | 26.2 | 24.8 | 49.7 | 43.3 | 46.4 | 43.5 |
| Ujenzi | 21.6 | 15.7 | 25.6 | 21.8 | 34.4 | 38.9 |
| Kilimo | 31.8 | 27.6 | 28.9 | 28.5 | 30.1 | 37.3 |
| Hoteli na migahawa | 13.0 | 16.3 | 2.5 | 4.4 | 0.9 | 25.1 |
| Shughuli binafsi | 13.1 | 14.7 | 17.7 | 20.7 | 21.8 | 24.7 |
| Viwanda | 6.3 | 0.1 | -8.2 | -4.9 | 8.3 | 5.1 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

**Kielelezo 2.2.6: Mgawanyo wa Mikopo Katika Shughuli za Kiuchumi**

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2. 3 Viwango vya Riba

Kwa ujumla, viwango vya riba vya mikopo na amana katika benki vilibaki tulivu mwezi Julai 2026. Kiwango cha jumla cha riba za mikopo kilipungua hadi asilimia 15.10 kutoka asilimia 15.22 mwezi Juni 2026, wakati kiwango cha riba kwa wateja wakubwa kiliongezeka kwa kiasi hadi asilimia 12.04 kutoka asilimia 11.93.

Kwa upande wa amana, riba ziliongezeka hadi asilimia 8.78 kutoka asilimia 8.69, wakati riba kwa wateja wakubwa zikipungua hadi asilimia 10.99 kutoka asilimia 11.17. Wigo kati ya riba za mikopo ya mwaka mmoja na riba za amana za mwaka mmoja uliongezeka kwa nukta 54 hadi asilimia 6.20, kutoka asilimia 5.66 mwezi Juni 2026 (Jedwali 2.3.1).

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo inayotolewa Benki za Biashara**

Asilimia

| | Jan-26 | Feb-26 | Mac-26 | Apr-26 | Mei-26 | Jun-26 | Jul-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.94 | 2.98 | 2.89 | 2.91 | 2.85 | 2.90 | 2.90 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.10 | 15.11 | 15.11 | 15.33 | 15.32 | 15.22 | 15.10 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 15.49 | 15.41 | 15.45 | 15.31 | 15.38 | 15.38 | 15.54 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.25 | 12.19 | 12.21 | 12.56 | 11.90 | 11.93 | 12.04 |
| Riba za amana -jumla | 8.33 | 8.32 | 8.33 | 8.54 | 8.43 | 8.69 | 8.78 |
| Riba za amana (miezi 12) | 9.70 | 9.82 | 9.60 | 9.81 | 10.17 | 9.72 | 9.34 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 11.74 | 11.48 | 11.57 | 11.37 | 11.25 | 11.17 | 10.99 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 5.79 | 5.59 | 5.85 | 5.50 | 5.22 | 5.66 | 6.20 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Masoko ya Fedha

### Soko la dhamana za Serikali

Mwezi Julai 2026, minada ya dhamana za Serikali ilipokea maombi makubwa kuliko zabuni zilizotangazwa, huku dhamana za muda mrefu zikiendelea kuvutia zaidi wawekezaji. Benki Kuu iliendesha minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi yenye thamani ya shilingi bilioni 580, kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya Serikali na kusimamia ukwasi. Zabuni zilikuwa shilingi bilioni 1,287.6, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 513.4 zilikubaliwa. Wastani wa riba ulipungua hadi asilimia 4.74 kutoka asilimia 4.83 mwezi Juni 2026 (Kielelezo 2.4.1).

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa Minada ya Dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Benki Kuu pia iliendesha minada mitatu ya hati fungani za Serikali za miaka 2, 10 na 20, zenye ukubwa wa zabuni wa jumla ya shilingi bilioni 684.9. Mahitaji katika minada yalifikia shilingi bilioni 1,466.2, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 641.9 zilikubaliwa.

Faida ya hati fungani ya miaka miwili ilibaki karibu na kiwango chake cha mwezi Juni 2026 kwa asilimia 8.40 ikilinganishwa na asilimia 8.36 mwezi uliotangulia. Hata hivyo, faida ya hati fungani za miaka 10 na 20 iliongezeka hadi asilimia 10.87 na asilimia 11.33, kutoka asilimia 10.39 na asilimia 10.43, mtawalia. Kutokana na mwenendo huo, kielelezo cha faida rejea, kilionesha kupanda zaidi, ambapo tofauti kati ya faida ya hati fungani ya miaka miwili na miaka 20 iliongezeka kwa pointi 86 na kufikia asilimia 2.93 (Jedwali 2.4.1).

**Jedwali 2.4.1: Faida Rejea ya Hati Fungani za Serikali**

| Aina ya Hati Fungani | Mnada uliopita | Jul-26 | Mabadiliko(bps) |
|---|---|---|---|
| Hati fungani ya miaka 2 | 8.36 | 8.4 | 4 |
| Hati fungani ya miaka 10 | 10.39 | 10.87 | 48 |
| Hati fungani ya miaka 20 | 10.39 | 11.33 | 90 |
| Tofauti kati ya hatifungani ya miaka 2 na 20 | 2.07 | 2.93 | 86 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya benki liliendelea kuwa njia kuu ya kugawa ukwasi wa shilingi baina ya mabenki, na hivyo kuimarisha utekelezaji wa sera ya fedha. Thamani ya miamala iliongezeka zaidi ya mara mbili hadi shilingi bilioni 5,627 mwezi Julai 2026, kutoka shilingi bilioni 2,508.7 mwezi Juni 2026, ambapo miamala ya siku 7 ilichangia asilimia 47.6 ya jumla ya miamala. Riba ya jumla katika soko la fedha baina ya benki iliongezeka kwa pointi 57 hadi asilimia 6.57, kutoka asilimia 6 (Kielelezo 2.4.2).

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la fedha za kigeni

Soko la fedha za kigeni baina ya mabenki liliendelea kuwa tulivu, likichagizwa na uwepo wa ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni uliotokana na mauzo makubwa ya dhahabu, mazao ya asili pamoja na shughuli za utalii. Mwezi Julai 2026, mauzo katika soko yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 227.1, ikilinganishwa na dola milioni 193.3 mwezi Juni 2026. Kuendana na Sera ya Ushiriki Katika Soko la Fedha za Kigeni, Benki Kuu iliuza dola za Marekani milioni 110.3, hasa kwa lengo la kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi katika soko (Kielelezo 2.4.3).

Katika kipindi hicho, shilingi ilipungua thamani dhidi ya dola ya Marekani kwa asilimia 0.8, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,653.52, kutoka shilingi 2,633.73 kwa dola moja mwezi Juni 2026. Kwa ulinganifu wa mwaka kwa mwaka, shilingi iliongezeka thamani kwa asilimia 0.5, ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 0.11 mwezi Julai 2025.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2. 5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Makusanyo ya mapato ya ndani mwezi Juni 2026 yalifikia shilingi bilioni 4,658.2 sawa na asilimia 5.4 juu ya lengo la mwezi husika. Serikali kuu ilikusanya shilingi bilioni 4,512.1 ikiwa ni sawa na asilimia 96.9 ya mapato ya ndani.

Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 3,733.2, sawa na asilimia 12.5 juu ya lengo la mwezi, ikiashiria athari chanya za maboresho yanayoendelea katika usimamizi wa kodi. Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 778.9, ikilinganishwa na lengo la makusanyo ya shilingi bilioni 953.8 (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Juni**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

Serikali imeendelea kuwianisha matumizi yake kuendana na mapato. Jumla ya matumizi ya Serikali mwezi Juni 2026 yalifikia shilingi bilioni 4,720.0, ambapo shilingi bilioni 2,797.9 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, huku shilingi bilioni 1,922.1 zikielekezwa kwenye miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Juni**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2026 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la taifa (linalojumuisha deni la Serikali la ndani na la nje, na deni la nje la sekta binafsi) lilifikia dola za Marekani milioni 50,782.1, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 0.07 ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa mwezi uliotangulia. Kati ya deni hilo, asilimia 70.7 ilikuwa deni la nje.

### Deni la Nje

Deni la nje (la sekta ya umma na sekta binafsi) liliongezeka kwa asilimia 0.2 kwa mwezi na kufikia dola za Marekani milioni 35,885.6 mwishoni mwa Julai 2026. Kati ya kiasi hicho, asilimia 83.7 ilikuwa deni la sekta ya umma, huku asilimia iliyobaki ikiwa ni deni la nje la sekta binafsi (Jedwali 2.6.1).

Katika mwezi huo, mikopo ya nje iliyopokelewa ilifikia dola za Marekani milioni 42.3, ambapo sehemu kubwa ilielekezwa kwa Serikali Kuu. Wakati huo huo, malipo ya deni la nje yalifikia

dola za Marekani milioni 122.0, ambapo dola za Marekani milioni 100.7 zilitumika kulipa deni la msingi.

Kwa kiasi kikubwa, mchanganuo wa deni la nje kwa kuzingatia wakopeshaji uliendelea kutobadilika, ambapo mashirika ya kimataifa yaliendelea kuwa wakopeshaji wakuu yakichangia asilimia 59.2 ya deni lote, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Shughuli za urari wa malipo na bajeti zilikuwa na sehemu kubwa zaidi ya deni hilo, zikifuatiwa na shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 65.3 ya deni lote, ikifuatiwa na sarafu ya umoja wa ulaya (Jedwali 2.6.3 na Jedwali 2.6.4).

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje Kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopaji | Jul-25r Kiasi | Jul-25r Mchango (%) | Jun-26r Kiasi | Jun-26r Mchango (%) | Jul-26p Kiasi | Jul-26p Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | 28,573.6 | 84.8 | 29,986.7 | 83.7 | 30,034.8 | 83.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 28,495.0 | 84.5 | 29,906.2 | 83.5 | 29,954.3 | 83.5 |
| Malimbikizo ya riba | 78.6 | 0.2 | 80.5 | 0.2 | 80.6 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 5,137.5 | 15.2 | 5,840.0 | 16.3 | 5,850.7 | 16.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,033.1 | 14.9 | 5,645.9 | 15.8 | 5,644.9 | 15.7 |
| Malimbikizo ya riba | 104.4 | 0.3 | 194.1 | 0.5 | 205.8 | 0.6 |
| Mashirika ya umma | 1.3 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1.3 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 33,712.4 | 100.0 | 35,826.6 | 100.0 | 35,885.6 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopeshaji | Jul-25r Kiasi | Jul-25r Mchango (%) | Jun-26r Kiasi | Jun-26r Mchango (%) | Jul-26p Kiasi | Jul-26p Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 19,894.2 | 59.0 | 21,200.0 | 59.2 | 21,256.8 | 59.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 19,872.1 | 58.9 | 21,175.9 | 59.1 | 21,232.4 | 59.2 |
| Malimbikizo ya riba | 22.1 | 0.1 | 24.1 | 0.1 | 24.4 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,536.8 | 4.6 | 1,547.0 | 4.3 | 1,557.7 | 4.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,458.2 | 4.3 | 1,466.5 | 4.1 | 1,477.1 | 4.1 |
| Malimbikizo ya riba | 78.6 | 0.2 | 80.5 | 0.2 | 80.6 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,597.7 | 34.4 | 12,435.6 | 34.7 | 12,427.3 | 34.6 |
| Deni ambalo halijalipwa | 11,537.7 | 34.2 | 12,302.4 | 34.3 | 12,283.2 | 34.2 |
| Malimbikizo ya riba | 60.0 | 0.2 | 133.1 | 0.4 | 144.1 | 0.4 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 683.6 | 2.0 | 644.0 | 1.8 | 643.8 | 1.8 |
| Deni ambalo halijalipwa | 661.4 | 2.0 | 607.2 | 1.7 | 606.4 | 1.7 |
| Malimbikizo ya riba | 22.2 | 0.1 | 36.9 | 0.1 | 37.4 | 0.1 |
| Jumla ya deni la nje | 33,712.4 | 100.0 | 35,826.6 | 100.0 | 35,885.6 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi.**

Asilimia

| Shughuli ya uchumi | Jul-25r | Jun-26r | Jul-26p |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 23.3 | 22.8 | 22.8 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.1 | 21.9 | 21.9 |
| Kilimo | 5.1 | 5.3 | 5.3 |
| Nishati na madini | 11.9 | 12.7 | 12.5 |
| Viwanda | 2.9 | 2.7 | 2.7 |
| Huduma za jamii na elimu | 19.8 | 19.4 | 19.5 |
| Fedha na bima | 3.6 | 4.2 | 4.2 |
| Utalii | 1.8 | 1.6 | 1.6 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 5.3 | 4.9 | 4.8 |
| Mengineyo | 5.1 | 4.6 | 4.6 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu.**

Asilimia

| Sarafu | Jul-25r | Jun-26r | Jul-26p |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 65.5 | 65.5 | 65.3 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 17.8 | 18.1 | 18.2 |
| Yuan ya China | 6.6 | 6.6 | 6.6 |
| Sarafu nyinginezo | 10.1 | 9.8 | 9.9 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Deni la Serikali la ndani liliongezeka kwa kiwango kidogo na kufikia shilingi bilioni 39,472.2 mwishoni mwa mwezi Julai 2026, ikilinganishwa na shilingi bilioni 39,325.8 mwezi uliotangulia. Ongezeko hilo lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na utoaji wa dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo (Kielelezo 2.6.1 na Jedwali 2.6.5). Benki za biashara na mifuko ya hifadhi ya jamii iliendelea kuwa wakopeshaji wakuu, ikichangia sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali (Jedwali 2.6.6).

**Kielelezo 2.6.1: Deni la ndani la Serikali Kuu**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa.

**Jedwali 2.6.5: Deni la ndani la Serikali kuu kwa Vyanzo vya Mikopo**

Shilingi Bilioni

| | Jul-25 | | Jun-26P | | Jul-26P | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nyenzo | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 32,048.0 | 85.8 | 33,314.4 | 84.7 | 35,530.5 | 90.0 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,075.7 | 5.6 | 1,757.5 | 4.5 | 1,778.7 | 4.5 |
| Hisa za serikali | 135.7 | 0.4 | 135.7 | 0.3 | 135.7 | 0.3 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 29,836.5 | 79.9 | 31,421.2 | 79.9 | 33,615.9 | 85.2 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,261.8 | 14.2 | 6,011.4 | 15.3 | 3,941.7 | 10.0 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 5,243.4 | 14.1 | 6,011.4 | 15.3 | 3,941.6 | 10.0 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 37,309.8 | 100.0 | 39,325.8 | 100.0 | 39,472.2 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

**Jedwali 2.6.6: Deni la ndani la Serikali Kuu kwa Kundi la Wakopeshaji**

Shilingi Bilioni

| | Jul-25 | | Jun-26P | | Jul-26P | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 10,176.3 | 28.8 | 11,320.8 | 28.8 | 11,450.6 | 29.0 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 6,799.3 | 19.2 | 7,197.1 | 18.3 | 6,819.7 | 17.3 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,328.8 | 26.4 | 10,399.0 | 26.4 | 10,491.4 | 26.6 |
| Kampuni za bima | 1,808.4 | 5.1 | 2,022.8 | 5.1 | 2,063.0 | 5.2 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 777.3 | 2.2 | 838.6 | 2.1 | 854.6 | 2.2 |
| Wengine | 6,461.3 | 18.3 | 7,547.4 | 19.2 | 7,792.9 | 19.7 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 35,351.4 | 100.0 | 39,325.8 | 100.0 | 39,472.2 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p, takwimu za awali; na "wengine" inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na wawekezaji wasio wakazi

Mwezi Julai 2026, Serikali ilikusanya shilingi bilioni 681.4 kutoka soko la ndani kupitia utoaji wa dhamana za Serikali, zikijumuisha shilingi bilioni 178.9 za dhamana za muda mfupi na shilingi bilioni 502.5 za dhamana za muda mrefu (Kielelezo 2.6.2).

Wakati huo huo, malipo ya deni la ndani yalifikia shilingi bilioni 566.4, ambapo shilingi bilioni 207.6 zilitumika kulipa deni la msingi na shilingi bilioni 358.8 zililipwa kama riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje ilikabiliwa na mazingira yasiyotabirika ya uchumi wa dunia katika mwaka ulioishia Julai 2026, yakichangiwa na kuendelea kwa migogoro ya kijiografia, kuyumba kwa masoko ya nishati, pamoja na gharama za juu za usafirishaji majini. Ongezeko la gharama za uagizaji na mvurugiko katika huduma za usafirishaji wa kimataifa vilisababisha shinikizo kwenye mwenendo wa sekta ya nje. Hata hivyo, bei nzuri ya dhahabu, kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii, pamoja na uhimilivu wa biashara ya kikanda, vilichangia kuongeza mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

Nakisi ya urari wa malipo iliongezeka kwa asilimia 21.3 na kufikia dola za Marekani milioni 2,395.3 mwaka ulioishia Julai 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,975.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 2.7.1). Nakisi inatokana na ongezeko la dola za Marekani milioni 3,018 za uagizaji wa bidhaa toka nje, likichangiwa na uwekezaji na mahitaji ya nishati, kiwango kilichozidi ongezeko la dola za Marekani milioni 2,828.3 za mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi (Jedwali 2.7.2).

Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa katika kiwango cha kuridhisha, ikifikia dola za Marekani milioni 6,199.6 mwishoni mwa Julai 2026, karibu sawa na kiwango kilichorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kiwango hicho cha akiba kilitosheleza kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.8, na hivyo kuendelea kuashiria uimara wa sekta ya nje (Kielelezo 2.7.1).

**Jedwali 2.7.1: Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali**

Dola za Marekani Milioni

| | | | | Mwaka ulioishia Julai | | | Mabadiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 | 2024 | 2025 | 2026p | ya asilimia |
| Urari wa bidhaa | -194.3 | -711.5 | -624.1 | -5,922.1 | -4,521.1 | -5,487.6 | 21.4 |
| Zilozouzwa nje* | 846.7 | 1,086.2 | 998.0 | 7,923.4 | 9,900.2 | 11,951.7 | 20.7 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,041.0 | 1,797.7 | 1,622.1 | 13,845.6 | 14,421.3 | 17,439.3 | 20.9 |
| Urari wa huduma | 516.03 | 398.4 | 620.7 | 4,176.3 | 4,094.7 | 4,665.9 | 14.0 |
| Mapato | 785.2 | 702.7 | 874.4 | 6,630.7 | 7,257.3 | 8,034.1 | 10.7 |
| Malipo | 269.1 | 304.4 | 253.6 | 2,454.4 | 3,162.6 | 3,368.1 | 6.5 |
| Urari wa bidhaa na huduma | 321.8 | -313.1 | -3.3 | -1,745.8 | -426.4 | -821.6 | 92.7 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,631.9 | 1,788.9 | 1,872.4 | 14,554.2 | 17,157.5 | 19,985.8 | 16.5 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,310.1 | 2,102.0 | 1,875.7 | 16,299.9 | 17,583.9 | 20,807.4 | 18.3 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -143.4 | -141.9 | -110.3 | -1,689.7 | -2,015.5 | -1,958.4 | -2.8 |
| Yaliyoingia | 38.0 | 80.9 | 54.7 | 334.3 | 303.9 | 376.2 | 23.8 |
| Yaliyotoka | 181.3 | 222.7 | 165.1 | 2,024.0 | 2,319.4 | 2,334.6 | 0.7 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 30.4 | 45.9 | 49.0 | 616.0 | 466.4 | 384.7 | -17.5 |
| Iliyoingia | 74.6 | 102.0 | 105.1 | 1,290.7 | 1,039.6 | 1,047.3 | 0.7 |
| ambapo Serikali | 0.0 | 0.0 | 0.8 | 129.0 | 97.4 | 23.0 | -76.3 |
| Iliyotoka | 44.2 | 56.2 | 56.1 | 674.7 | 573.2 | 662.6 | 15.6 |
| Urari wa bidhaa, huduma na uhamisho mali | 208.8 | -409.1 | -64.6 | -2,819.5 | -1,975.4 | -2,395.3 | 21.3 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali *Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.7.1: Akiba ya Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: LHS inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

## Mauzo ya nje

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 16.5 na kufikia dola za Marekani milioni 19,985.8 mwaka ulioishia Julai 2026, kutoka kiwango kilichorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2025. Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mauzo ya bidhaa nje ya nchi pamoja na mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji.

Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 20.7, kufikia dola za Marekani milioni 11,951.7, yakichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku na kahawa. Mauzo ya dhahabu yaliongezeka kwa asilimia 37.4 kufikia dola za Marekani milioni 5,670.7 mwaka ulioishia Julai 2026, yakichangiwa na bei nzuri katika soko la Dunia. Dhahabu ilichangia asilimia 47.4 ya mapato yote yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi, na hivyo kuendelea kuimarisha nafasi yake kama chanzo kikuu cha fedha za kigeni nchini.

Mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa asilimia 46.0 na kufikia dola za Marekani milioni 2,215.5, yakichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za chuma na bidhaa zake, bidhaa za kioo pamoja na nguo, sambamba na uwepo endelevu wa mahitaji kikanda.

Mauzo ya bidhaa asilia yaliongezeka kwa asilimia 14.9 na kufikia dola za Marekani milioni 1,628.8, yakiongozwa na tumbaku na kahawa.

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 998.0 mwezi Julai 2026, kutoka dola za Marekani milioni 846.7 mwezi kama huo 2025 (Kielelezo 2.7.2).

**Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 8,034.1 kutoka dola za Marekani milioni 7,257.3, yakichangiwa na utalii, na usafirishaji bidhaa. Mapato ya huduma za usafirishaji yaliongezeka kwa asilimia 29.7 hadi dola za Marekani milioni 3,221.5, yakiakisi kuongezeka kwa mapato ya usafirishaji wa mizigo kufuatia ongezeko la mizigo inayovuka mipaka.

Mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 1.6 na kufikia dola za Marekani milioni 4,292.8. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 874.4 mwezi Julai 2026, kutoka dola za Marekani milioni 785.2 mwezi Julai 2025 (Kielelezo 2.7.3).

**Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Huduma nyinginezo zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za fedha, mawasiliano ya simu, komputa na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili, huduma za serikali, huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

## Uagizaji wa Bidhaa na Huduma

Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 18.3 na kufikia dola za Marekani milioni 20,807.4 mwaka ulioishia Julai 2026, ikilinganishwa na kiasi kilichorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa mtaji, bidhaa za viwandani, mafuta ya petroli, na usafirishaji wa mizigo, sambamba na kuimarika kwa uwekezaji na upanuzi wa viwanda. Uagizaji wa bidhaa uliongezeka hadi dola za Marekani milioni 17,439.3, kutoka dola za Marekani milioni 14,421.3, ukiongozwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa mtaji na bidhaa za kati.

Uagizaji wa mafuta meupe yaliyosafishwa, ambao ulichangia asilimia 18.9 ya jumla ya gharama za uagizaji wa bidhaa, uliongezeka kwa asilimia 42.3 na kufikia dola za Marekani milioni 3,296.8, ukiakisi ongekezo la bei za mafuta katika soko la Dunia na uendelevu wa mahitaji ya ndani. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa uliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,622.1 mwezi Julai 2026, kutoka dola za Marekani milioni 1,041.0 mwezi Julai 2025 (Kielelezo 2.7.4).

**Kielelezo 2.7.4: Ulinganifu wa Uagizaji wa bidhaa na huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi p inamaanisha takwimu za awali.

Malipo ya huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 3,368.1 kutoka dola za Marekani milioni 3,162.6, yakichangiwa zaidi na ongezeko la malipo ya usafirishaji wa mizigo, sambamba na ongezeko la uagizaji wa bidhaa na kupanda kwa gharama za usafirishaji wa mizigo majini. Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 253.6 mwezi Julai 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 269.1 mwezi Julai 2025 (Kielelezo 2.7.5).

**Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo:Ukokotoaji wa Benki kuu ya Tanzania

Tanbihi: Huduma nyingine zinajumuisha ujenzi, bima, huduma za kifedha, mawasiliano ya simu, kompyuta na taarifa, ada za matumizi ya mali miliki ya kiakili,huduma za kiserikali,huduma binafsi, na huduma nyingine za kibiashara.

Nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi ilipungua hadi dola za Marekani milioni 1,958.4, kutoka dola za Marekani milioni 2,015.5, ikichangiwa zaidi na kupungua kwa malipo ya riba kwa wasiokuwa wakazi. Kwa upande mwingine, ziada ya urari wa uhamisho wa mali za kawaida ilipungua hadi dola za Marekani milioni 384.7, kutoka dola za Marekani milioni 466.4, hali iliyotokana zaidi na kupungua kwa uhamisho wa fedha binafsi.

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi ilipungua hadi dola za Marekani milioni 110.3 mwezi Julai 2026, kutoka dola za Marekani milioni 143.4. Vilevile, ziada ya urari ya uhamisho wa mali wa kawaida iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 49.0, kutoka dola za Marekani milioni 30.4.

# 3.0 Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

## 3.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei wa mwaka uliongezeka hadi asilimia 6.0 mwezi Julai 2026, kutoka asilimia 4.1 mwezi Julai 2025 (Jedwali 3.1.1 na Kielelezo 3.1.1). Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei ya chakula, pamoja

na kuongezeka kwa gharama za usafiri kufuatia kupanda kwa bei ya mafuta (Kielelezo 3.1.2).

Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula uliendelea kubaki katika kiwango cha chini, ukishuka hadi asilimia 1.9 mwezi Julai 2026 kutoka asilimia 3.9 mwezi Julai 2025. Kupungua huku kulionekana zaidi katika makundi ya mavazi na viatu pamoja na makazi, huduma za maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo (Jedwali 3.1.1). Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mfumuko wa bei wa jumla ulipungua kasi na kufikia asilimia 0.1 mwezi Julai 2026, ikilinganishwa na asilimia 1.0 iliyorekodiwa mwezi Julai 2025.

**Kielelezo 3.1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei**

Asilimia

| Makundi ya Fahirisi | Mizania | Badiliko Mwezi kwa Mwezi | | | Badiliko kwa Mwaka | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 |
| Vyakula na vinywaji visivyo na kileo | 41.9 | 0.1 | 1.7 | 0.6 | 4.9 | 10.3 | 10.9 |
| Vinywaji vyenye vileo, tumbaku na madawa ya binadamu | 0.2 | 4.9 | 1.1 | 2.9 | 3.4 | 5.5 | 3.5 |
| Mavazi na viatu | 6.3 | 0.1 | 0.0 | 0.2 | 5.1 | 1.4 | 1.4 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyingine | 25.8 | 0.4 | 0.5 | -0.9 | 3.4 | 1.8 | 0.5 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na matengenezo ya kawaida ya nyumba | 4.8 | 0.5 | 1.3 | 0.7 | 4.3 | 3.7 | 4.0 |
| Afya | 1.3 | 0.1 | 0.0 | 0.3 | 1.6 | 0.7 | 0.9 |
| Uchukuzi | 9.1 | -0.1 | 0.1 | -0.7 | 2.3 | 5.3 | 4.7 |
| Taarifa na mawasiliano | 4.2 | 0.0 | 0.0 | 0.9 | 2.7 | -0.6 | 0.3 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.1 | -0.8 | 0.0 | -0.2 | 4.3 | 2.0 | 2.7 |
| Elimu | 1.6 | 1.7 | 0.0 | 0.0 | 3.8 | 2.0 | 0.3 |
| Huduma za migahawa na malazi | 1.4 | 1.0 | 0.0 | -0.2 | 1.6 | 7.4 | 6.2 |
| Bima na huduma za fedha | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Huduma binafsi, ulinzi wa kijamii na bidhaa na huduma mbalimbali | 1.7 | 0.1 | 0.0 | 0.9 | 5.0 | 0.8 | 1.6 |
| Mfumuko wa bei wa jumla | 100.0 | 0.2 | 1.0 | 0.1 | 4.1 | 6.0 | 6.0 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula | 40.5 | 0.1 | 1.7 | 0.6 | 4.3 | 10.5 | 11.1 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula | 59.5 | 0.3 | 0.4 | -0.3 | 3.9 | 2.5 | 1.9 |

Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

**Kielelezo 3.1.1: Mfumuko wa Bei wa Mwaka**

Kizio: Julai 2022 =100




Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

**Kielelezo 3.1.2: Wastani wa Bei za Rejareja za Mafuta ya Petroli kwa Mwezi**




Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## 3.2 Bajeti ya Serikali

Rasilimali za Serikali, zinazojumuisha mapato ya ndani na misaada, zilifikia shilingi bilioni 188.1 mwezi Julai 2026, sawa na asilimia 74.1 ya lengo la mwezi. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 179.6, sawa na asilimia 89.4 ya lengo, huku misaada ikichangia shilingi bilioni 8.5.

Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 152.9, sawa na asilimia 87.1 ya lengo. Utendaji huu ulitokana na makusanyo ya kuridhisha ya kodi ya mapato, kodi ya ongezeko la thamani, pamoja na ushuru wa bidhaa .

Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 26.7 yakizidi lengo kwa asilimia 5.5, yakichangiwa na kuimarika kwa makusanyo yatokanayo na ada na tozo (Kielelezo 3.2.1).

**Kielelezo 3.2.1: Mapato ya Serikali**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar

Tanbihi: Kodi nyingine zinahusisha tozo za hoteli, tozo za wasindikiza wageni, stampu za tozo, tozo za huduma za viwanja vya ndege na bandari, tozo za maendeleo ya barabara na petroli

Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 304.5 mwezi Julai 2026, ambapo, shilingi bilioni 195.7 zilitumika kugharamia matumizi ya maendeleo na shilingi bilioni 108.7 zilitumika kugharamia matumizi ya kawaida. Nakisi ya shilingi bilioni 116.4 iligharamiwa na mikopo ya ndani (Kielelezo 3.2.2).

**Kielelezo 3.2.2: Matumizi ya Serikali**

Shilingi Bilioni




Chanzo:Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar

Tanbihi: Matumizi mengine yanahusisha uhamisho wa fedha, malipo ya riba ya deni la ndani, huduma za mfuko mkuu wa serikali na tozo zingine.

## 3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Urari wa malipo uliendelea kuwa na ziada, ingawa ziada hiyo ilipungua hadi dola za Marekani milioni 771.1 mwaka ulioishia Julai 2026, kutoka dola za Marekani milioni 848.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 (Jedwali 3.3.1). Kupungua kwa ziada kunaakisi ukuaji wa asilimia 64.0 wa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, ambao ulizidi ongezeko la asilimia 22.4 la mauzo ya bidhaa na huduma.

**Jedwali 3.3.1: Urari wa Malipo**

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26 | Mwaka unaoishia Julai 2025 | Mwaka unaoishia Julai $2026^{p}$ | Ongezeko/ Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa bidhaa (Halisi) | -43.2 | -196.8 | -198.8 | -511.5 | -902.8 | 76.5 |
| Zilizouzwa nje | 1.7 | 3.3 | 3.3 | 32.1 | 70.6 | --- |
| Zilizonunuliwa kutoka nje | 44.9 | 200.1 | 202.1 | 543.6 | 973.4 | 79.1 |
| Urari wa huduma (halisi) | 171.0 | 121.8 | 181.4 | 1,348.5 | 1,659.0 | 23.0 |
| Mapato | 178.9 | 126.6 | 196.0 | 1,449.8 | 1,743.3 | 20.2 |
| Malipo | 7.9 | 4.8 | 14.6 | 101.3 | 84.3 | -16.8 |
| Urari wa bidhaa na huduma (halisi) | 127.7 | -75.0 | -17.4 | 837.0 | 756.2 | -9.7 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 180.6 | 129.9 | 199.4 | 1,481.9 | 1,813.9 | 22.4 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 52.8 | 204.9 | 216.7 | 644.9 | 1,057.7 | 64.0 |
| Urari wa mapato ya msingi (halisi) | 0.3 | 1.9 | 2.2 | 10.4 | 12.3 | 18.2 |
| Yaliyoingia | 0.3 | 2.0 | 2.4 | 14.8 | 14.0 | -5.0 |
| Yaliyotoka | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 4.4 | 1.8 | -59.9 |
| Urari wa uhamishaji Mali (halisi) | 0.0 | 0.5 | 0.7 | 1.2 | 2.6 | 121.0 |
| Iliyoingia | 0.1 | 0.6 | 0.7 | 2.4 | 3.3 | 33.5 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 1.3 | 0.6 | -48.8 |
| Urari wa Bidhaa,huduma na uhamishaji mali | 128.0 | -72.6 | -14.5 | 848.6 | 771.1 | -9.1 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, benki na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Tanbihi: p inaashiria Takwimu za awali; fob, 'Mzigo ndani ya chombo.

### Mauzo ya nje

Mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka kwa asilimia 22.4 na kufikia dola za Marekani milioni 1,813.9, yakichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma, hususan utalii (Jedwali 3.3.1). Mauzo ya bidhaa nayo yaliongezeka kwa kiasi kikubwa, yakichangiwa na ongezeko la mauzo ya bidhaa asilia, hususan karafuu (Jedwali 3.3.2).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, mauzo ya bidhaa na huduma yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 199.4 mwezi Julai 2026, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 180.6 zilizorekodiwa mwezi Julai 2025.

**Jedwali 3.3.2: Uuzaji wa Bidhaa**

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Uniti | Jul-25 | Jun-26 | Jul-26p | Mwaka unaoishia Julai 2025 | Mwaka unaoishia Julai 2026p | Ongezeko/Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mauzo ya nje ya bidhaa za asili | | | | | | | |
| Karafuu | | | | | | | |
| Thamani | 000' ya Dola ya Marekani | 123.8 | 815.8 | 824.0 | 3,574.0 | 42,888.4 | --- |
| Kiasi | 000' kwa Tani | 0.0 | 0.7 | 0.8 | 0.8 | 7.8 | --- |
| Bei kwa Unit | Dola ya Marekani/Tani | 3,374.2 | 1,089.1 | 1,100.0 | 46,198.8 | 61,200.8 | 32.5 |
| Mauzo ya nje ya bidhaa zisizo za asili Mwani | | | | | | | |
| Thamani | 000' ya Dola ya Marekani | 277.9 | 151.2 | 152.7 | 3,363.2 | 1,356.1 | -59.7 |
| Kiasi | Dola ya Marekani/Tani | 0.5 | 0.3 | 0.3 | 6.0 | 2.5 | -58.9 |
| Bei kwa Unit | Dola ya Marekani/Tani | 548.8 | 495.5 | 500.5 | 6,472.7 | 5,779.2 | -10.7 |
| Bidhaa za Viwandani | 000' ya Dola ya Marekani | 892.8 | 1,716.9 | 1,734.0 | 15,991.3 | 12,627.7 | -21.0 |
| Bidhaa za samaki | 000' ya Dola ya Marekani | 47.2 | 322.9 | 326.2 | 1,023.4 | 1,315.8 | 28.6 |
| Mauzo ya nje ya nchini kwa bidhaa nyingine | 000' ya Dola ya Marekani | 348.4 | 303.8 | 306.9 | 8,152.1 | 12,406.0 | 52.2 |
| Jumla Ndogo | 000' ya Dola ya Marekani | 1,566.3 | 2,494.8 | 2,519.7 | 28,530.0 | 27,705.6 | -2.9 |
| Jumla Kuu | 000' ya Dola ya Marekani | 1,690.1 | 3,310.6 | 3,343.7 | 32,104.0 | 70,593.9 | --- |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## Uagizaji wa bidhaa na huduma

Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa asilimia 64.0 na kufikia dola za Marekani milioni 1,057.7 mwaka ulioishia Julai 2026 (Jedwali 3.3.1), ukichangiwa na ongezeko la uagizaji wa bidhaa mtaji na bidhaa za matumizi. Uagizaji wa bidhaa mtaji uliongezeka kwa kiwango kikubwa, ukichangiwa zaidi na ongezeko la uagizaji wa mishine na mitambo mbalimbali, pamoja na vifaa vya usafiri viwandani. Ongezeko la uagizaji wa bidhaa za matumizi uliakisi uagizaji wa bidhaa za matumizi na vifaa vya usafiri visivyo vya viwandani (Jedwali 3.3.3).

Kwa ulinganifu wa mwezi kwa mwezi, uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 216.7 mwezi Julai 2026, kutoka dola za Marekani milioni 52.8 mwezi Julai 2025.

# Viambatisho

## Jedwali A1: Viashiria vya Kiuchumi

| | | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024[r] | 2025[p] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukuaji wa Pato la Taifa na Mfumuko wa bei | | | | | | | | | |
| 1. 1Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika | Asilimia | 4.4 | 8.5 | 8.1 | 7.4 | 9.4 | 10.5 | 10.2 | na |
| 1.2 Ukuaji halisi wa Pato ta Taifa | Asilimia | 7.0 | 6.9 | | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 | 6.0 |
| 1.3 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika | '000' sh | 2,356.5 | 2,479.3 | 2,597.7 | 2,705.4 | 2,854.1 | 3,058.8 | 3,234.9 | na |
| 1.4 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika | Dola ya Marekani | 1,041.0 | 1,083.5 | 1,126.7 | 1,171.6 | 1,233.1 | 1,263.1 | 1,239.2 | na |
| 1.5 Kasi ya Upandaji wa Bei | Asilimia | 3.5 | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 | 3.3 |
| 1.6 Uwiano wa Akiba kwa Pato halisi la Taifa | Asilimia | 18.7 | 18.6 | 16.5 | 17.3 | 19.7 | 21.2 | 25.8 | na |
| Takwimu za Kifedha na Riba | | | | | | | | | |
| 2.1 Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | Asilimia | 4.5 | 9.6 | 5.7 | 15.5 | 11.6 | 14.1 | 11.1 | 24.7 |
| 2.2.Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | Asilimia | 3.8 | 11.8 | 8.2 | 17.6 | 12.1 | 11.9 | 9.2 | 28.5 |
| 2.3 Ukuaji va Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | Asilimia | 5.1 | 13.7 | 7.5 | 23.1 | 7.5 | 8.7 | 11.2 | 30.2 |
| 2.4 Ukuaji Fedha ya msingi (M0) | Asilimia | 0.6 | 6.8 | -4.0 | 17.3 | 15.8 | 3.7 | 19.1 | 20.7 |
| 2.5 Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi | Asilimia | 4.9 | 11.1 | 3.1 | 10.0 | 22.5 | 17.3 | 12.4 | 23.6 |
| 2.6 Uwiano wa Mikopo kwa Sekta Binafsi kwa pato la taifa[1] | Asilimia | 14.3 | 14.6 | 14.0 | 14.3 | 16.0 | 17.0 | 17.4 | 21.6 |
| 2.7 Uwiano wa Mikopo kwa sekta binafSikwa mikopo yote | Asilimia | 79.8 | 83.5 | 77.7 | 74.4 | 72.9 | 73.9 | 75.9 | 77.9 |
| 2.8 Riba za Amana za miezi 12 | Asilimia | 8.8 | 8.8 | 8.3 | 8.3 | 8.5 | 8.7 | 9.2 | 9.6 |
| 2.9 Riba za dhamana za serkali kwa ujumla | Asilimia | 6.4 | 7.7 | 4.4 | 4.8 | 4.7 | 7.3 | 10.7 | 8.7 |
| 2.10 Riba ya mikopo ya muda mrefu hadi miaka mitano (3-5 years) | Asilimia | 17.4 | 16.6 | 16.2 | 16.0 | 15.7 | 15.6 | 15.3 | 14.4 |
| Mizania ya Malipo na Nchi za Nje | | | | | | | | | |
| 3.1 Bidhaa Ziizouzwa Nje | Dola ya Marekani | 4,292.7 | 5,377.6 | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 | 10,293.6 |
| 3.2.Bidhaa Zilazoagizwa kutoka Nje ya Nchi | Dola ya Marekani | -8,519.7 | -8,615.2 | -7,831.7 | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,195.6 | -14,787.7 |
| 3.3.Urari wa Biashara | Dola ya Marekani | -4,227.0 | -3,237.5 | -1,460.0 | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,074.0 | -4,494.2 |
| 3.4.Urari wa Malipo ya Kawaida | Dola ya Marekani | -2,308.7 | -1,340.2 | -1,458.5 | -2,374.3 | -5,482.2 | -2,960.6 | -2,379.8 | -2,015.2 |
| 3.5 Urari wa malipo yote | Dola ya Marekani | -784.0 | 587.0 | -764.9 | 1,852.1 | -988.4 | 52.3 | 70.1 | 968.9 |
| 3.6 Akiba ya Fedha za Kigeni | Dola ya Marekani | 5,044.6 | 5,567.6 | 4,767.7 | 6,386.0 | 5,177.2 | 5,450.1 | 5,546.9 | 6,329.0 |
| 3.7 Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | Miezi | 4.9 | 6.4 | 5.6 | 6.6 | 4.7 | 4.5 | 4.5 | 4.9 |
| 3. 8 Kiwango cha kubadili fedha: | | | | | | | | | |
| Wastani wa mwaka | Thamani ya Tsh/Dola | 2,263.8 | 2,288.2 | 2,294.1 | 2,297.8 | 2,303.1 | 2,382.1 | 2,597.4 | 2,537.6 |
| Mwisho wa kipindi | Thamani ya Tsh/Dola | 2,281.2 | 2,287.9 | 2,298.5 | 2,297.6 | 2,308.9 | 2,501.4 | 2,374.7 | 2,450.2 |
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Mwenendo wa Mapato na Matumizi | | | | | | | | | |
| 4.1 Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 14.8 | 14.3 | 15.0 | 13.7 | 14.9 | 15.0 | 14.7 | 15.6 |
| 4.2 Uwiano wa misaada kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 0.8 | 0.4 | 0.7 | 0.5 | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 0.4 |
| 4.3 Uwiano wa Matumiazi ya kawaida kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 10.2 | 10.7 | 10.1 | 9.9 | 9.8 | 11.0 | 10.8 | 11.9 |
| 4.4 Uwiano wa matumizi ya maendeleo kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 6.6 | 6.5 | 7.1 | 7.8 | 9.2 | 7.4 | 7.2 | 6.9 |
| 4.5 Uwiano wa nakisi isiyo jumuisha misaada kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | -2.1 | -2.9 | -2.2 | -4.0 | -4.1 | -3.4 | -3.3 | -3.2 |
| 4.6 Uwiano wa nakisi ya Jumla kwa Pato la Taita[1,2] | Asilimia | -1.9 | -3.3 | -1.9 | -4.0 | -3.6 | -3.1 | -3.1 | -3.0 |
| Deni la nje | Dola Milion | 20,503.0 | 21,920.9 | 22,952.7 | 25,519.3 | 27,832.5 | 30,252.7 | 31,950.9 | 34,765.3 |
| 5.1 Mikopo ilyopokelewa | Dola Milion | 18,765.1 | 20,029.3 | 20,958.4 | 23,250.9 | 25,392.8 | 27,889.3 | 30,416.1 | 34,053.0 |
| 5.2 Riba ambayo haijaipwa | Dola Milion | 1,737.9 | 1,891.7 | 1,994.3 | 2,268.4 | 2,439.7 | 2,363.4 | 1,534.8 | 712.3 |

Chanzo:Wizara ya Fedha; Benki Kuu ya Tanzania; na Mamlaka ya Mapato Tanzania

Tanbihi: [1]Imetolewa kwa kuzingatia Pato la Tifa kwa bei za miaka husika; [2]inajumuisha misaada, matumizi yaliyochelewa (expenditure float) n.a-haipatikani, p- ni takwimu za muda.

## Jedwali A2: Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali – Tanzania Bara

Shilingi Milioni

| | Bajeti ya | Julai 2025 - Juni 2026 | | Juni 2026 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2025/26 | Makadirio | Halisi | Makadirio | Halisi |
| Mapato ya ndani (yakijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa) | 40,466,131.4 | 40,466,131.4 | 41,930,401.7 | 4,419,685.4 | 4,658,209.3 |
| Mapato ya Serikali Kuu | 36,857,734.1 | 38,785,624.7 | 40,323,733.0 | 4,273,554.7 | 4,512,078.6 |
| Mapato yatokanayo na kodi | 32,175,999.8 | 32,175,999.8 | 34,579,237.5 | 3,319,803.6 | 3,733,208.7 |
| Ushuru wa forodha | 11,562,965.6 | 11,562,965.6 | 12,559,150.7 | 995,620.2 | 1,213,277.2 |
| Kodi ya bidhaa na huduma | 7,016,470.7 | 7,016,470.7 | 6,492,281.7 | 684,616.4 | 587,519.9 |
| Kodi ya mapato | 11,367,876.5 | 11,268,555.1 | 13,220,630.9 | 1,436,366.6 | 1,702,890.5 |
| Kodi nyingine | 4,887,699.8 | 2,328,008.4 | 2,307,174.3 | 203,200.3 | 229,521.2 |
| Mapato yasiyotokana na kodi | 4,681,734.3 | 6,609,624.9 | 5,744,495.5 | 953,751.2 | 778,869.8 |
| Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680,506.8 | 1,680,506.8 | 1,606,668.7 | 146,130.7 | 146,130.7 |
| Jumla ya matumizi[1] | 48,774,989.1 | 48,774,988.6 | 48,450,981.8 | 4,979,798.8 | 4,720,004.3 |
| Matumizi ya kawaida | 31,281,255.8 | 31,169,595.9 | 31,393,743.2 | 2,965,416.5 | 2,797,927.3 |
| Mishahara | 10,917,466.8 | 13,121,530.2 | 13,279,276.9 | 1,119,767.1 | 1,163,080.0 |
| Malipo ya riba za mikopo | 6,493,715.4 | 6,938,880.5 | 5,605,312.0 | 644,023.8 | 597,384.9 |
| Ya ndani | 3,697,288.1 | 3,856,359.9 | 3,690,648.5 | 332,083.8 | 465,316.4 |
| Ya nje | 2,796,427.3 | 3,082,520.6 | 1,914,663.5 | 311,940.1 | 132,068.5 |
| Matumizi mengine ya kawaida | 7,088,606.6 | 11,109,185.2 | 12,509,154.3 | 1,201,625.5 | 1,037,462.5 |
| Matumizi ya maendeleo | 17,493,733.4 | 17,605,392.8 | 17,057,238.6 | 2,014,382.3 | 1,922,077.0 |
| Fedha za ndani | 12,117,828.4 | 12,253,013.3 | 13,044,234.2 | 1,309,440.3 | 1,200,912.9 |
| Fedha za nje | 5,375,904.9 | 5,352,379.5 | 4,013,004.4 | 704,942.0 | 721,164.1 |
| Nakisi ya bajeti bila ya misaada | -8,308,857.7 | -8,308,857.2 | -6,520,580.1 | -560,113.3 | -61,795.0 |
| Misaada | 1,069,884.4 | 1,052,678.8 | 917,555.0 | 188,820.1 | 118,689.9 |
| Ya bajeti | 113,796.3 | 113,796.3 | 0.0 | 113,796.3 | 0.0 |
| Ya miradi | 846,976.2 | 779,943.3 | 837,744.0 | 69,275.5 | 113,637.2 |
| Ya kisekta | 109,111.9 | 158,939.3 | 79,811.0 | 5,748.3 | 5,052.8 |
| Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada | -6,401,157.9 | -7,256,178.4 | -5,603,025.1 | -371,293.2 | 56,894.9 |
| Marekebisho (Adjustments to cash and other items (net)) | 0.0 | 0.0 | -544,639.1 | 0.0 | -419,514.3 |
| Balansi ya jumla | -7,238,973.3 | -7,256,178.4 | -6,147,664.2 | -371,293.2 | -362,619.4 |
| Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti | 7,238,973.3 | 7,256,178.4 | 6,147,664.2 | 371,293.2 | 362,619.4 |
| Ufadhili kutoka nje halisi | 4,286,343.5 | 3,715,721.0 | 2,705,924.6 | 654,947.9 | 477,421.6 |
| Mikopo | 5,966,414.1 | 8,325,509.8 | 6,064,529.0 | 1,257,091.8 | 886,268.8 |
| Mikopo ya bajeti | 1,627,221.4 | 1,371,698.4 | 1,143,646.0 | 627,173.7 | 0.0 |
| Mikopo ya miradi | 4,339,192.6 | 6,953,811.4 | 4,920,883.0 | 629,918.1 | 886,268.8 |
| ambayo: Mikopo ya masharti ya kibiashara | 2,629,011.8 | 2,629,012.5 | 1,894,321.5 | 0.0 | 283,794.7 |
| Mikopo ya kisekta | 80,624.2 | 88,698.0 | 68,887.9 | 0.0 | 0.0 |
| Marejesho ya mitaji ya mikopo ya nje | -4,389,706.5 | -4,698,486.8 | -3,427,492.3 | -602,144.0 | -408,847.2 |
| Ufadhili wa ndani halisi[2] | 2,952,629.8 | 3,540,457.4 | 3,441,739.6 | -283,654.7 | -114,802.2 |
| Mikopo kutoka benki na vyanzo vingine | 2,952,629.8 | 3,540,457.4 | 3,441,739.6 | -283,654.7 | -114,802.2 |
| Mikopo ya benki | 2,466,103.9 | 2,957,070.9 | 1,543,967.6 | -236,914.9 | -242,567.7 |
| Mikopo toka vyanzo vingine (baada ya marejesho ya mitaji ya miko | 486,526.0 | 583,386.5 | 1,897,772.0 | -46,739.8 | 127,765.5 |
| Mikopo ya ndani (rollover) | 3,325,556.5 | 3,340,372.6 | 3,286,053.0 | 1,311,536.8 | 909,926.8 |
| Kulipa mitaji ya mikopo ya ndani | -3,325,556.5 | -3,340,372.6 | -3,286,053.0 | -1,311,536.8 | -909,926.8 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

Tanbihi: [1] Haijajumuisha marejesho ya mitaji ya mikopo na matumizi yaliyochelewa (expenditure float); [2] Thamani chanya ina maana ya ufadhili, na thamani hasi ina maana ya malipo au ongezeko la amana

**Jedwali A3: Tathmini za Amana**

| Kipengele | Jul-25 | Ago-25 | Sep-25 | Okt-25 | Nov-25 | Des-25 | Jan-26 | Feb-26 | Mac-26 | Apr-26 | Mei-26 | Jun-26 | Jul-26 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 15,726.1 | 15,766.0 | 15,896.7 | 15,715.4 | 16,298.6 | 15,286.5 | 15,950.0 | 15,749.5 | 15,245.6 | 14,553.5 | 13,309.2 | 13,449.0 | 14,646.0 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 13,884.0 | 13,933.2 | 14,467.3 | 13,334.3 | 13,892.1 | 13,707.3 | 13,987.7 | 14,089.2 | 13,916.0 | 13,066.6 | 12,634.5 | 13,077.5 | 14,562.1 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,842.1 | 1,832.8 | 1,429.3 | 2,381.1 | 2,406.5 | 1,579.1 | 1,962.3 | 1,660.3 | 1,329.6 | 1,486.8 | 674.7 | 371.6 | 83.9 |
| Rasilimali halisi za ndani | 40,565.0 | 41,689.9 | 41,957.4 | 44,073.3 | 44,560.0 | 45,702.6 | 46,155.7 | 47,319.8 | 49,001.1 | 50,538.4 | 53,494.7 | 56,170.4 | 56,763.8 |
| Madai ya ndani | 52,548.3 | 54,561.2 | 54,854.2 | 56,509.3 | 57,629.3 | 57,229.9 | 57,872.1 | 58,896.1 | 59,877.3 | 61,759.8 | 63,283.0 | 65,928.9 | 65,896.2 |
| Madai halisi kwa Serikali Kuu | 11,576.1 | 13,030.4 | 12,854.4 | 14,122.4 | 14,243.8 | 12,626.9 | 12,700.8 | 12,841.9 | 12,660.8 | 13,840.5 | 14,248.3 | 14,005.8 | 12,122.6 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 40,972.2 | 41,530.9 | 41,999.9 | 42,386.9 | 43,385.5 | 44,603.1 | 45,171.4 | 46,054.2 | 47,216.5 | 47,919.3 | 49,034.6 | 51,923.1 | 53,773.6 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 56,291.1 | 57,455.9 | 57,854.0 | 59,788.6 | 60,858.6 | 60,989.1 | 62,105.7 | 63,069.3 | 64,246.7 | 65,091.9 | 66,803.8 | 69,619.4 | 71,409.8 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 8,122.1 | 8,036.4 | 7,730.8 | 8,410.1 | 8,545.0 | 8,492.1 | 8,102.1 | 8,151.8 | 8,078.3 | 8,107.1 | 8,444.4 | 8,824.5 | 8,933.6 |
| Amana za hundi | 26,155.4 | 27,442.8 | 28,352.1 | 29,032.2 | 28,992.7 | 29,049.1 | 30,023.9 | 30,521.3 | 31,188.5 | 32,154.3 | 33,066.8 | 34,753.3 | 35,932.6 |
| Amana za akiba na muda maalumu | 22,013.5 | 21,976.7 | 21,771.2 | 22,346.4 | 23,320.9 | 23,447.8 | 23,979.7 | 24,396.2 | 24,979.9 | 24,830.5 | 25,292.6 | 26,041.5 | 26,543.6 |
| Fedha taslim (M0) | 13,423.8 | 13,537.9 | 13,717.6 | 15,068.7 | 15,135.7 | 14,508.3 | 15,225.1 | 14,990.0 | 14,998.9 | 15,670.5 | 15,640.3 | 16,738.8 | 16,188.3 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 56,291.1 | 57,455.9 | 57,854.0 | 59,788.6 | 60,858.6 | 60,989.1 | 62,105.7 | 63,069.3 | 64,246.7 | 65,091.9 | 66,803.8 | 69,619.4 | 71,409.8 |
| Amana za fedha za kigeni (FCD) | 13,653.2 | 13,696.3 | 13,337.2 | 13,882.1 | 14,056.5 | 13,255.7 | 14,103.2 | 14,569.7 | 14,998.4 | 14,989.0 | 15,428.5 | 15,365.4 | 16,771.0 |
| *Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)* | *5,369.8* | *5,560.2* | *5,462.9* | *5,662.4* | *5,768.4* | *5,410.2* | *5,600.8* | *5,730.6* | *5,809.8* | *5,764.1* | *5,913.1* | *5,853.2* | *6,339.0* |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 42,637.9 | 43,759.6 | 44,516.8 | 45,906.5 | 46,802.2 | 47,733.4 | 48,002.5 | 48,499.6 | 49,248.3 | 50,102.9 | 51,375.3 | 54,254.1 | 54,638.9 |
| Amana za akiba na muda maalum zilizo katika shilingi ya Kitanzania | 16,406.3 | 16,357.2 | 16,600.4 | 16,848.4 | 17,618.1 | 17,919.5 | 18,229.5 | 18,541.9 | 19,071.4 | 18,951.4 | 19,122.7 | 19,982.0 | 19,984.5 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 26,231.6 | 27,402.4 | 27,916.4 | 29,058.1 | 29,184.1 | 29,813.8 | 29,773.0 | 29,957.7 | 30,176.9 | 31,151.6 | 32,252.6 | 34,272.0 | 34,654.4 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 8,122.1 | 8,036.4 | 7,730.8 | 8,410.1 | 8,545.0 | 8,492.1 | 8,102.1 | 8,151.8 | 8,078.3 | 8,107.1 | 8,444.4 | 8,824.5 | 8,933.6 |
| Amana za hundi | 18,109.4 | 19,366.0 | 20,185.6 | 20,648.0 | 20,639.0 | 21,321.7 | 21,670.9 | 21,805.9 | 22,098.5 | 23,044.5 | 23,808.2 | 25,447.5 | 25,720.8 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali A4: Muundo wa Viwango vya Riba

Asilimia

| | 2025 | | | | | | 2026 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipengele | Jul | Ago | Sep | Okt | Nov | Des | Jan | Feb | Mac | Apr | Mei | Jun | Jul |
| A: Riba za mikopo/amana zilizo katika shilingi | | | | | | | | | | | | | |
| 1. Riba katika soko la fedha baina ya mabenki | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 1 (*Overnight*) | 6.62 | 6.15 | 6.29 | 6.45 | 6.08 | 6.00 | 6.13 | 6.01 | 6.17 | 6.15 | 5.94 | 5.53 | 5.92 |
| Siku 2-7 | 7.43 | 6.52 | 6.43 | 6.29 | 6.19 | 6.30 | 6.34 | 6.31 | 6.25 | 6.18 | 5.96 | 5.90 | 6.23 |
| Siku 8-14 | 7.57 | 6.71 | 6.93 | 6.92 | 6.84 | 6.26 | 6.74 | 6.83 | 6.53 | 6.33 | 6.48 | 6.46 | 6.90 |
| Siku 15-30 | 7.12 | 6.87 | 7.35 | 7.07 | 7.23 | 6.40 | 7.06 | 6.96 | 6.85 | 6.79 | 6.58 | 6.64 | 7.31 |
| Siku 31-60 | 8.53 | 6.90 | 7.50 | 7.28 | 7.00 | 7.20 | 7.23 | 7.00 | 7.20 | 6.92 | 6.79 | 6.70 | 6.90 |
| Siku 61-90 | 9.14 | 9.14 | 9.14 | 9.14 | 7.00 | 8.11 | 9.96 | 7.00 | 8.50 | 7.12 | 6.79 | 6.84 | 6.82 |
| Siku 91-180 | 11.39 | 7.00 | 7.00 | 9.75 | 8.89 | 8.89 | 6.75 | 7.00 | 8.07 | 8.77 | 7.27 | 7.07 | 6.92 |
| Zaidi ya siku 180 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 12.00 | 12.00 | 12.00 | 12.00 | 12.00 | 12.00 |
| Riba ya jumla | 7.35 | 6.48 | 6.45 | 6.38 | 6.30 | 6.29 | 6.40 | 6.34 | 6.32 | 6.26 | 6.14 | 6.00 | 6.57 |
| 2. Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.25 | 7.25 | 7.25 | 7.75 |
| 3. Riba ya mikopo ya muda mfupi toka kwa | 5.30 | 5.30 | 4.79 | 4.79 | 4.79 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 6.25 |
| 4. Riba ya mikopo ya muda mfupi kwa | 5.77 | 5.78 | 5.76 | 5.76 | 5.77 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 5.75 | 6.25 |
| 5. Riba ya dhamana za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 35 | 6.50 | 6.50 | 6.20 | 5.94 | 5.64 | 5.38 | 5.36 | 4.75 | 4.20 | 3.81 | 3.23 | 2.82 | 2.34 |
| Siku 91 | 7.46 | 7.36 | 6.81 | 6.21 | 6.08 | 5.93 | 5.73 | 4.97 | 4.23 | 4.02 | 3.78 | 3.56 | 3.40 |
| Siku 182 | 8.24 | 7.46 | 6.56 | 6.41 | 5.92 | 5.91 | 5.85 | 5.85 | 5.69 | 5.46 | 5.23 | 4.98 | 4.74 |
| Siku 364 | 8.13 | 6.79 | 5.99 | 6.00 | 6.45 | 6.24 | 6.21 | 6.20 | 5.80 | 5.72 | 5.63 | 6.65 | 7.07 |
| Riba ya jumla | 8.13 | 6.83 | 6.03 | 6.27 | 6.25 | 5.87 | 5.89 | 5.68 | 5.21 | 5.06 | 4.74 | 4.83 | 4.74 |
| 6. Riba za hati fungani za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 12.17 | 12.17 | 12.17 | 10.05 | 10.05 | 10.05 | 10.05 | 10.05 | 8.36 | 8.36 | 8.36 | 8.36 | 8.40 |
| Miaka mitano | 13.18 | 13.18 | 12.48 | 12.48 | 10.54 | 10.54 | 10.54 | 10.54 | 10.54 | 9.54 | 9.54 | 9.54 | 9.54 |
| Miaka saba | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 13.74 | 13.74 | 13.74 | 12.45 | 12.45 | 12.45 | 11.30 | 11.30 | 11.30 | 9.40 | 9.40 | 10.39 | 10.87 |
| Miaka kumi na tano | 14.63 | 13.91 | 13.91 | 13.91 | 12.08 | 12.08 | 12.08 | 10.78 | 10.78 | 10.78 | 10.39 | 10.39 | 10.39 |
| Miaka ishirini | 14.50 | 14.50 | 13.55 | 13.55 | 13.55 | 12.02 | 12.02 | 12.02 | 10.71 | 10.71 | 10.43 | 10.43 | 11.33 |
| Miaka ishirini na tano | 14.80 | 14.42 | 13.19 | 13.19 | 13.19 | 13.19 | 13.19 | 11.99 | 11.99 | 11.99 | 11.99 | 11.89 | 11.89 |
| 7. Riba inayotumika kutathmini dhamana | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 |
| 8. Riba za amana za akiba | 2.90 | 2.90 | 2.92 | 2.93 | 2.88 | 3.02 | 2.94 | 2.98 | 2.89 | 2.91 | 2.85 | 2.90 | 2.90 |
| 9. Riba za jumla za amana za muda maalum | 8.83 | 8.61 | 8.50 | 8.36 | 8.54 | 8.36 | 8.33 | 8.32 | 8.33 | 8.54 | 8.43 | 8.69 | 8.78 |
| Mwezi 1 | 11.50 | 10.70 | 9.65 | 9.10 | 9.31 | 9.35 | 8.96 | 9.10 | 8.65 | 9.06 | 8.34 | 9.28 | 9.51 |
| Miezi 2 | 10.75 | 10.07 | 9.28 | 10.09 | 9.67 | 9.34 | 9.56 | 9.16 | 9.34 | 9.67 | 8.65 | 9.84 | 10.13 |
| Miezi 3 | 10.19 | 8.59 | 9.61 | 9.38 | 9.42 | 9.70 | 9.43 | 9.03 | 9.56 | 9.01 | 10.52 | 9.96 | 9.61 |
| Miezi 6 | 10.28 | 10.44 | 10.12 | 10.06 | 10.01 | 9.96 | 10.20 | 10.26 | 10.51 | 10.35 | 9.87 | 10.46 | 10.54 |
| Miezi 12 | 9.88 | 9.99 | 9.84 | 9.21 | 10.02 | 9.58 | 9.70 | 9.82 | 9.60 | 9.81 | 10.17 | 9.72 | 9.34 |
| Miezi 24 | 5.99 | 7.16 | 7.63 | 7.05 | 7.92 | 7.21 | 7.11 | 7.35 | 7.03 | 8.20 | 7.69 | 7.91 | 7.91 |
| 10. Riba za amana kwa wateja wakubwa | 10.72 | 10.99 | 11.05 | 11.22 | 11.67 | 11.66 | 11.74 | 11.48 | 11.57 | 11.37 | 11.25 | 11.17 | 10.99 |
| 11. Wastani wa riba za mikopo | 15.16 | 15.07 | 15.18 | 15.19 | 15.27 | 15.24 | 15.10 | 15.11 | 15.11 | 15.33 | 15.32 | 15.22 | 15.10 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 15.51 | 15.64 | 15.52 | 15.50 | 15.53 | 15.46 | 15.49 | 15.41 | 15.45 | 15.31 | 15.38 | 15.38 | 15.54 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 16.41 | 16.45 | 16.26 | 16.42 | 16.42 | 16.42 | 16.73 | 16.70 | 16.53 | 17.19 | 17.11 | 17.10 | 16.51 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 15.22 | 15.01 | 15.19 | 15.13 | 15.18 | 15.43 | 14.97 | 15.27 | 15.31 | 15.63 | 15.60 | 15.19 | 15.11 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 14.39 | 14.02 | 14.26 | 14.24 | 14.43 | 14.29 | 14.05 | 13.96 | 13.95 | 14.56 | 14.43 | 14.38 | 14.44 |
| Muda mrefu (Zaidi ya Miaka 5) | 14.28 | 14.22 | 14.66 | 14.68 | 14.79 | 14.61 | 14.24 | 14.20 | 14.30 | 13.96 | 14.08 | 14.03 | 13.92 |
| 12. Riba za mikopo kwa wateja wakubwa | 12.56 | 12.72 | 12.84 | 12.40 | 12.61 | 12.38 | 12.25 | 12.19 | 12.21 | 12.56 | 11.90 | 11.93 | 12.04 |
| B: Fedha za kigeni | | | | | | | | | | | | | |
| 1. Riba za amana | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 0.83 | 0.93 | 0.98 | 1.75 | 0.57 | 0.87 | 0.77 | 0.70 | 1.22 | 1.68 | 1.06 | 1.64 | 1.65 |
| Riba za jumla za amana za muda maalum | 3.75 | 4.11 | 3.94 | 4.17 | 4.03 | 3.67 | 4.18 | 4.29 | 4.26 | 4.41 | 4.47 | 4.30 | 4.11 |
| Mwezi 1 | 2.50 | 2.46 | 2.46 | 2.44 | 2.45 | 2.45 | 2.52 | 2.45 | 2.47 | 3.42 | 2.52 | 2.49 | 2.49 |
| Miezi 2 | 3.02 | 4.02 | 4.98 | 4.93 | 6.12 | 2.96 | 4.97 | 4.85 | 4.84 | 3.91 | 4.05 | 5.02 | 4.72 |
| Miezi 3 | 4.31 | 4.98 | 2.56 | 4.55 | 2.87 | 4.92 | 4.95 | 4.94 | 4.69 | 4.87 | 5.03 | 4.72 | 3.94 |
| Miezi 6 | 4.94 | 4.60 | 5.10 | 5.05 | 5.25 | 4.82 | 4.66 | 4.80 | 4.97 | 5.03 | 5.14 | 4.69 | 4.76 |
| 9 months | 4.00 | 4.47 | 4.61 | 3.86 | 3.47 | 3.19 | 3.82 | 4.43 | 4.35 | 4.83 | 5.59 | 4.57 | 4.65 |
| Miezi 12 | 8.82 | 8.59 | 8.43 | 8.71 | 8.52 | 8.61 | 8.57 | 8.61 | 8.70 | 8.96 | 8.72 | 9.03 | 8.88 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 9.91 | 9.89 | 9.89 | 9.88 | 9.89 | 9.91 | 10.00 | 10.00 | 10.00 | 10.07 | 9.95 | 9.99 | 10.02 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 8.23 | 8.11 | 7.49 | 7.73 | 7.65 | 7.68 | 7.68 | 7.72 | 7.69 | 8.82 | 7.88 | 8.31 | 8.13 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 7.03 | 7.16 | 7.25 | 7.43 | 7.49 | 8.31 | 8.35 | 8.23 | 8.19 | 8.64 | 7.79 | 8.84 | 8.81 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 9.42 | 9.30 | 9.16 | 9.23 | 9.30 | 8.50 | 8.64 | 8.83 | 9.09 | 9.19 | 9.08 | 9.09 | 8.70 |
| Muda mrefu (zaidi ya miaka 5) | 9.52 | 8.49 | 8.35 | 9.28 | 8.28 | 8.66 | 8.17 | 8.28 | 8.50 | 8.09 | 8.88 | 8.92 | 8.76 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali A5: Mizania ya Malipo ya Nje**

Dola za Marekami Milioni

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| A. Urari wa malipo ya kawaida | -2,374.3 | -5,482.2 | -2,960.6 | -2,379.8 | -2,049.4 |
| Bidhaa: zilizouzwa nje ya nchi (f.o.b) | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 | 10,262.9 |
| Bidhaa asilia | 627.9 | 766.5 | 953.3 | 1,473.3 | 1,491.9 |
| Bidhaa zisizo asilia | 5,763.0 | 6,058.4 | 6,321.6 | 7,228.8 | 8,464.5 |
| kati ya hizo: Dhahabu | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,419.6 | 4,753.9 |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 419.6 | 306.6 |
| Bidhaa: zilizoagizwa kutoka nje ya nchi (f.o.b) | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,195.6 | -14,787.7 |
| *Urari wa biashara ya bidhaa* | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,074.0 | -4,524.8 |
| Huduma: mapato | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,231.7 | 6,846.8 | 7,477.5 |
| Usafirishaji | 1,558.1 | 1,872.0 | 2,333.4 | 2,353.4 | 2,647.6 |
| Utalii | 1,310.3 | 2,527.8 | 3,373.8 | 3,903.1 | 4,410.6 |
| Nyingine | 249.3 | 362.2 | 524.4 | 590.3 | 419.2 |
| Huduma: malipo | -1,607.0 | -2,465.4 | -2,395.9 | -2,795.0 | -3,241.8 |
| Usafirishaji | -806.4 | -1,378.4 | -1,326.4 | -1,411.9 | -1,467.3 |
| Utalii | -196.2 | -357.5 | -477.2 | -522.3 | -715.5 |
| Nyingine | -604.4 | -729.5 | -592.3 | -860.9 | -1,059.1 |
| *Urari wa biashara ya huduma* | 1,510.7 | 2,296.6 | 3,835.9 | 4,051.7 | 4,235.7 |
| *Urari wa biashara ya bidhaa na huduma* | -1,736.4 | -4,688.3 | -2,196.5 | -1,022.3 | -289.1 |
| Mapato ya vitega uchumi: yaliyoingia | 102.5 | 183.9 | 301.2 | 311.7 | 306.2 |
| Malipo ya vitega uchumi: yaliyotoka | -1,294.2 | -1,577.1 | -1,797.7 | -2,199.2 | -2,356.3 |
| *Urari wa mapato ya vitega uchumi* | -1,191.6 | -1,393.2 | -1,496.6 | -1,887.4 | -2,050.1 |
| *Urari wa bidhaa, huduma na mapato ya vitega uchumi* | -2,928.0 | -6,081.5 | -3,693.1 | -2,909.7 | -2,339.2 |
| Mapato ya uhamisho mali wa kawaida: yaliyoingia | 640.1 | 716.5 | 1,280.9 | 1,177.4 | 899.1 |
| Serikali | 104.7 | 76.4 | 131.0 | 139.2 | 19.7 |
| Taasisi za zisizo za serikali | 535.4 | 640.2 | 1,150.0 | 1,038.3 | 879.4 |
| Malipo ya uhamisho mali wa kawaida: yaliyotoka | -86.4 | -117.2 | -548.4 | -647.5 | -609.2 |
| *Urari wa uhamisho mali wa kawaida* | 553.7 | 599.3 | 732.5 | 529.9 | 289.9 |
| B. Urari wa uhamisho mitaji | 412.1 | 274.0 | 223.4 | 318.7 | 348.9 |
| Uhamisho wa mitaji: ulioingia | 412.1 | 274.0 | 223.4 | 318.7 | 348.9 |
| Serikali | 346.8 | 208.7 | 158.0 | 253.3 | 289.8 |
| Taasisi za zisizo za serikali | 65.3 | 65.3 | 65.3 | 65.3 | 59.1 |
| Uhamisho wa mitaji: uliotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla, A na B | -1,962.1 | -5,208.2 | -2,737.2 | -2,061.1 | -1,700.5 |
| C. Urari katika uwekezaji | 4,037.1 | 3,634.7 | 3,629.9 | 1,857.4 | 2,750.0 |
| *Uwekezaji wa moja kwa moja* | 1,190.5 | 1,437.6 | 1,648.9 | 1,656.0 | 1,850.4 |
| *Uwekezaji wa hisa* | -7.9 | 24.6 | 13.9 | 10.6 | 82.3 |
| *Uwekezaji mwingine* | 2,854.5 | 2,172.5 | 1,967.1 | 190.7 | 817.3 |
| Mali (assets) | -89.8 | 193.0 | -749.6 | -924.6 | -417.3 |
| Madeni (liabilities) | 2,944.3 | 1,979.6 | 2,716.6 | 1,115.3 | 1,234.6 |
| *Jumla, makundi A hadi C* | 2,074.9 | -1,573.4 | 892.7 | -203.8 | 1,049.5 |
| D. Makosa na masahihisho | -222.8 | 585.0 | -850.8 | 273.9 | -80.6 |
| *Urari wa malipo yote* | 1,852.1 | -988.4 | 41.9 | 70.1 | 968.9 |
| E. Akiba ya fedha za kigeni | -1,852.1 | 988.4 | -41.9 | -70.1 | -968.9 |
| | | | | | |
| Vipengele vya kumbukumbu | | | | | |
| Uwiano wa urari wa malipo ya kawaida kwa pato la taifa | -3.4 | -7.1 | -3.7 | -2.9 | -2.2 |
| Akiba ya fedha za kigeni | 6,386.0 | 5,177.2 | 5,450.1 | 5,546.9 | 6,329.0 |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi ya uagizaji wa bidhaa nje) | 6.6 | 4.7 | 4.5 | 4.5 | 4.9 |
| Kiwango cha kubadilisha fedha (mwisho wa kipindi) | 2,297.6 | 2,308.9 | 2,501.4 | 2,374.7 | 2,450.2 |
| Kiwango cha kubadilisha fedha (kwa wastani kwa mwaka) | 2,297.8 | 2,303.0 | 2,382.1 | 2,597.4 | 2,537.6 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania.

Tanbihi: p inaashiria takwimu za awali; “---“, badiliko linalozidi asilimia 100; f.o.b Mzigo ndani ya chombo

**Jedwali A6: Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi**

Dola za Marekani Milioni

| | Mwaka ulioishia Julai | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026p |
| Bidhaa asilia | 750.6 | 782.5 | 1,074.4 | 1,418.0 | 1,628.8 |
| Korosho | 230.0 | 164.2 | 225.6 | 527.6 | 479.3 |
| Karafuu | 62.3 | 38.3 | 32.3 | 3.2 | 28.4 |
| Kahawa | 162.6 | 207.3 | 210.9 | 337.5 | 396.0 |
| Pamba | 92.8 | 100.5 | 109.4 | 56.9 | 91.2 |
| Katani | 21.5 | 25.1 | 19.9 | 31.0 | 34.2 |
| Chai | 31.3 | 32.4 | 20.9 | 18.7 | 11.2 |
| Tumbaku | 149.9 | 214.6 | 455.3 | 443.0 | 588.6 |
| Bidhaa zisizo asilia | 5,935.0 | 6,299.1 | 6,454.7 | 8,090.2 | 9,984.7 |
| Madini | 3,208.8 | 3,578.9 | 3,692.5 | 4,830.5 | 6,395.4 |
| Dhahabu | 2,707.1 | 2,939.0 | 3,148.0 | 4,127.1 | 5,670.7 |
| Almasi | 29.2 | 46.8 | 42.9 | 46.5 | 50.2 |
| Tanzanite | 23.2 | 25.2 | 22.8 | 17.3 | 15.9 |
| Madini mengineyo | 449.4 | 567.9 | 478.9 | 639.6 | 658.7 |
| Bidhaa za mbogamboga na maua | 363.6 | 296.5 | 437.0 | 488.0 | 482.1 |
| Mbogamboga | 287.3 | 203.9 | 329.8 | 369.3 | 339.9 |
| Maua | 25.7 | 24.3 | 27.9 | 28.4 | 31.1 |
| Matunda | 22.1 | 35.6 | 47.0 | 54.9 | 69.0 |
| Nyingine | 28.5 | 32.7 | 32.3 | 35.3 | 42.2 |
| Bidhaa za viwandani | 1,324.2 | 1,423.4 | 1,293.8 | 1,517.3 | 2,215.5 |
| ambapo Saruji | 50.9 | 62.0 | 37.8 | 45.1 | 60.6 |
| Bidhaa za Ceramic | 49.0 | 37.9 | 21.8 | 28.9 | 29.3 |
| Vipodozi | 42.2 | 46.5 | 38.0 | 48.9 | 53.2 |
| Mafuta ya Kula | 18.9 | 17.1 | 24.0 | 44.4 | 59.4 |
| Mbolea | 79.8 | 115.1 | 35.8 | 72.8 | 52.0 |
| Vyombo vya Kioo | 41.5 | 53.4 | 75.8 | 113.8 | 139.5 |
| Chuma na vyuma | 103.7 | 90.8 | 77.7 | 99.7 | 156.0 |
| Karatasi na bidhaa zake | 67.8 | 34.8 | 21.0 | 41.5 | 60.4 |
| Vitu vya Plastiki | 40.1 | 38.7 | 40.2 | 51.3 | 56.7 |
| Nguo na Vitambaa | 118.9 | 95.9 | 78.6 | 94.7 | 103.0 |
| Nafaka | 365.6 | 219.5 | 154.9 | 383.0 | 172.2 |
| Mahindi | 117.6 | 59.2 | 29.8 | 185.5 | 98.3 |
| Mchele | 238.8 | 147.2 | 115.0 | 182.7 | 71.9 |
| Nafaka nyinginezo | 9.2 | 13.1 | 10.2 | 14.7 | 2.0 |
| Samaki na mazao ya samaki | 180.8 | 159.6 | 178.2 | 166.0 | 178.4 |
| Mafuta ya mbegu | 162.6 | 281.4 | 294.6 | 282.3 | 176.9 |
| Bidhaa nyingine za mauzo ya nje | 214.5 | 200.7 | 217.0 | 238.6 | 210.1 |
| Kati ya hizo: Maharage | 40.9 | 51.9 | 12.3 | 1.9 | 12.5 |
| Mbao na bidhaa za mbao | 112.7 | 77.5 | 89.0 | 80.3 | 73.4 |
| Kakao | 26.5 | 29.3 | 76.2 | 105.2 | 68.5 |
| Mimea | 3.7 | 12.5 | 9.6 | 9.6 | 19.3 |
| Ngozi na bidhaa za ngozi | 5.3 | 4.1 | 4.4 | 5.3 | 4.7 |
| Mauzo ya ndani ya nchi kwenda nje | 6,685.5 | 7,081.5 | 7,529.1 | 9,508.2 | 11,613.5 |
| Bidhaa zilizosafirishwa tena nje (Re-export | 114.9 | 139.2 | 186.6 | 184.5 | 154.0 |
| Mauzo yasiyorekodiwa | 397.8 | 414.2 | 389.1 | 363.0 | 316.2 |
| Jumla ya mauzo nje | 7,083.4 | 7,495.8 | 7,918.2 | 9,871.2 | 11,929.7 |

Chanzo: Mamlaka ya mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali A7: Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

Dola za Marekani Milioni

| | Mwaka ulioishia Julai | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026p |
| Bidhaa za kukuza mtaji | 2,082.2 | 2,951.8 | 2,768.5 | 3,056.3 | 4,021.6 |
| Mashine na mitambo | 935.4 | 1,284.5 | 1,083.7 | 1,095.2 | 1,440.1 |
